# AFYA NA MAZINGIRA

## Kutofuatwa kwa sheria ya mazingira kunavyohatarisha afya za wananchi



LUNDO la takataka

NA WARIOBA IGOMBE.

MKOA wa Morogoro ni miongoni mwa mikoa nchini, ambayo wananchi wake wanatamani kuona siku moja nao unakuwa ni jiji kama ilivyo kwa wananchi wa mkoa wa Dar es Salaam ,Mwanza ,Arusha, Tanga na Dodoma ambayo ni majiji.

Lakini ndoto za wananchi hawa wa Morogoro inaweza kushindwa kutimia kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo mlundikano wa taka ngumu na hii ni kwa sababu ya sheria ya mazingira mkoani humo maarufu,kwa jina la Mji kasoro Bahari kutofuatwa.

Kwa mjibu wa sheria ya usimamizi wa mazingira ya mwaka 2004 kifungu Na 118(1) kinachohusu taka ngumu ni kuwa Mamlaka ya serikali za mitaa, itatenga vituo vya kuweka taka kwa muda ambavyo vitatumika kukusanyia taka ngumu katika majiji, manispaa, miji au maeneo mengine.

Sheria hiyo ineleza kwamba kabla ya mamlaka ya serikali za mitaa haijatenga eneo kuwa kituo cha kuweka taka ngumu, kwa muda kwa madhumuni ya kukusanya taka hizo, mamlaka hiyo itafanya tathmini ya athari kwa jamii, afya na mazingira.

Lengo la kufanya tathimini hiyo ni kuhakikisha kuwa eneo hilo linatosha kwa ukubwa na liko mbali na makazi ya watu, kuhakikisha uondoaji wa mara kwa mara wa taka ngumu unafanyika ili kuepuka kero na itahakikisha kwamba eneo hilo limewekewa uzio na linalindwa, ili kuzuia watu wasiohusika kuingia.

Mbali sheria hii kutaka uondoaji wa taka ufanyike mara kwa mara kuepuka kero, kutoka kwa wananchi na pia kuhakikisha kuwa eneo lililotengwa linakuwa na uzio ili kuzuia wasiohusika kuingia, sheria hii inaonekana kutofuatwa hali iliyosababisha kuwepo kwa malalamiko kutoka wa wananchi wa Manispaa ya Morogoro.

Katikati ya Mji wa Morogoro, maeneo ya Uwanja wa Jamhuri karibu na Bwalo la Umwema linalomilikiwa na Jeshi la Kungenga Taifa(JKT), kuna eneo limetengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka kabla ya kuzizoa na kuzipeleka sehemu maalumu inayohusika.

Eneo hili kuwekwa pipa maalumu kwa ya kuhifadhia taka ngum, hususan za plastiki lakini kutokana na wingi wa taka zinazokusanywa maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro hasa Kata ya Boma, pipa hili limezidiwa hali inayofanya wakusanya taka kupitia vikundi vyao kumwaga taka hizo chini.

Kitendo hiki cha kumwaga taka chini kimekuwa kukisababisha mludikano mkubwa wa taka, hasa ngumu zikiwemo za plastiki hali ambayo imesababisha malalamiko ya wananchi wakidai kuwa mlundikano huo ni hatari kiafya.

Jackson Abel mkazi wa Morogoro, anasema mlundiano wa taka katika eneo hilo unasambabishwa na uzembe wa viongozi wa serikali waliopewa jukumu la kusimamia sheria za mazingira, hivyo kuleta athari kwa jamii.

"Eneo hili kuna shule hivyo wanafunzi wanapita kila siku, kuna njia ambayo watu wa rika zote tunapita hapa, lakini pia kuna biashra ya vyakula kwa hiyo mlundikano huu wa taka hauleti picha nzuri kwa jamii,"anasema Abel.

Abel anasema sheria za mazingira inayohusu taka ngumu zipo wazi, lakini hazifuatwi na ndiyo sababu ya kuwepo kwa mludikano huo, ambapo amewaomba viongozi wa Manispaa kuliangalia suala hilo kwa jicho la tatu kwani bila hivyo kunaweza kusababisha kuwepo kwa magonjwa ya mlipuko.

Naye Sabina Juma, anasema mludikano wa taka eno hilo ni hatari hususan kwa watoto, ambao wamekuwa wakiptia eneo hilo kila siku kwenda shule kwani baadhi yao wamekuwa wakiingia katika eneo hilo, kwa ajili ya kuokota chupa za kuchezea.

"Eneo hili ni hatari kwa kuwa kuna taka mbalimbali, zikiwemo chupa na mifuko ya plastiki na chupa za kawaida, hivyo kitendo cha watoto kupita eneo hili ni hatari, kwani baadhi yao huingia katika mlundiano wa kata hizi kutafuta vitu vya kuchezea,"anasema Sabina.

Inocenti Albert mkazi wa Forest Manispaa ya Morogoro, anasema uwepo wa taka hizo kwa muda mrefu pasipo kuondolewa na mamlaka husika kumesababisha eneo hilo kuwa na harufu mbaya, ambapo ameiomba Manispaa ya Morogoro kulifunga eneo hilo na kutafuta sehemu nyingine kwa ajili ya kuhifadhi taka hizo.

### UDHIBITI USAFI WA MAZINGIRA

Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa Taka na Usafi Manispaa ya Morogoro Samwel Subi, anakiri kuwa maeneo mengi ya Manispaa ya Morogoro, yanakabiliwa na kero ya mlundikano wa taka na kwamba hali hiyo inasababishwa na uhaba wa magari.

Subi anasema Manispaa ya Morogoro, inakabiliwa na changamoto ya magari ya kubebea taka kutoka sehemu zilizotengwa kwa ajili ya kukusanya na kisha kuzoa taka hizo na kwenda kuzimwaga eneo lililotayarishwa kwa ajili ya kumwaga taka.

Anasema kwamba Manispaa ya Morogoro, kuna vikundi vya usafi ambavyo vimekuwa vikitoa huduma ya kukusanya taka na kuzipeleka katika mapipa makubwa ya kuhifadhia taka, kwa muda ambapo baada ya muda mapipa hayo hubwebwa na magari kwa lengo la kwenda kuzimwaga taka hizo.

"Tumeweka mapipa makubwa ya kuhifadhia taka kila kona ya Manipaa hii, hasa maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu, lakini changamoto iliyopo ni magari yetu ya kubebea taka ni mabovu na ndiyo sababu ya kusababisha mludikano wa taka hasa ngumu zikiwemo za plastiki,"anasema.

Anasema kwamba awali kulikuwa na kampuni iliyokuwa ikihusika na uzoaji wa taka, lakini baada ya mkataba kuisha mwenye kampuni hiyo hakutaka kuendelea na kazi hiyo kwani aliona gharama ya uendeshaji ni kubwa ukilinganisha na faidia anayoipata.

GHARAMA ZA UZOAJI TAKA

Kwa mujibu wa Subi ni kuwa kila kaya hutakiwa kulipa sh. 1000 kwa ajili ya uzoaji taka katika makazi yao, huku wafanyabiashara kama vile sokoni au genge muhusika kutakiwa kilipa sh. 6,000, huku wafanyabiashara wakubwa wakitakiwa kulipa sh. 80,000 kwa mwezi.

Anasema kitendo cha kila kaya kulipa sh. 1,000 kwa ajili ya uzoaji taka kwa mwezi haikidhi gharama za uendeshaji wa zoezi la uzoaji wa taka na ndiyo sababu za kuwepo kwa malalamiko ya wananchi juu ya suala zima la mlundikano wa taka.

Mkuu wa kitengo cha udhibiti wa taka na usafi anasema hayo yote yamesababishwa na sheria za Manispaa hiyo inayohusu ada ya taka, kwani shera hiyo inataka kila kaya kulipa sh. 1,000 kwa mwezi kwa ajili ya taka, hivyo kushindwa kukidhi gharama za uendeshaji.

Subi anakiri kwamba kutokana na changamoto hiyo ya uhaba wa magari, Manispaa ya Morogoro inaonekana haifuati kikamilifu sheria ya mazingira ya mwaka 2004, hasa katikae kipengele cha kutenga maeneo ya kuhifadhia taka hususan taka ngumu kwa muda,maeneo yasiyo karibu na watu.

"Sheria hii ya mazingira inataka uondoaji wa taka ufanyike mara kwa mara ili kuepuka kero kutoka kwa wananchi na pia kuhakikisha kuwa eneo lililotengwa linakuwa na uzio na pia linalindwa, ili kuzuia wasiohusika kuingia lakini kwa Manispaa yetu sheria hii ni kama haitekelezwi kikamilifu,"alisema Subi.

> **"Tumeweka mapipa makubwa ya kuhifadhia taka kila kona ya Manipaa hii, hasa maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu, lakini changamoto iliyopo ni magari yetu ya kubebea taka ni mabovu na ndiyo sababu ya kusababisha mludikano wa taka hasa ngumu zikiwemo za plastiki,"**
> **Samwel Sub, Mkuu wa Kitengo cha Udhibiti wa Taka na Usafi Manispaa ya Morogoro.**

### HALI ILIVYO

Subi anasema Manispaa ya Morogoro huzalisha tani 337 za taka kwa siku, kutoka maeneo mbalimbali hususan maeneo ya masoko, biashara ya vyakula, hoteli, ikiwa ni pamoja na kwenye makazi ya watu pamoja na maeneo ya biashara za magenge.

Mbali na changamoto ya ubovu wa magari ya kubeba taka,uhaba wa magari hayo, Subi anakiri kuwa Manispaa hiyo haifuati ipasavyo sheria ya mazingira, kwa baadhi ya vipengele kama kuweka uzio maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kukusanya taka kwa muda.

### SULUHISHO LA TATIZO

Subi asasema ili kukabiliana na changamoto ya mlundikano wa taka, Manispaa hiyo imeanza taratibu za kufanya malekebisho ya sheria za uzoaji taka, ili kila kaya badala ya kutoa sh. 1,000 kwa mwezi iwe inatoa sh. 3,000 kwa mwezi kwani kutasaidia kukidhi gharama za uendeshaji.

Anasema suala la taka za plastiki ni mtambuka hivyo wananchi wanatakiwa kuelimishwa juu ya utupaji ovyo wa taka hizo, ili kuepuka athari zake na kwamba upo utaratibu unaandaliwa wa kuweka vikusanya taka maeneo mbalimbali ya Manispaa hiyo, kwa lengo la kutenganisha taka za aina zote.

### ATHARI ZA MLUNDIKANO WA TAKA

Daktari Bingwa wa Majonjwa ya ndani katika Hosptali ya Rufaa Mkoa wa Morogoro Celement Lubeya, anasema kuna athari nyingi za kiafya, ambazo mtu anaweza kuzipata endapo ataishi katika mazingira yenye mlundikano wa taka.

Dk. Lubeya anataka athari hizo kuwa ni magonjwa ya mlipuko kama vile kipindupindu, kuhara, homa ya matumbo hasa katika kipindi hiki cha mvua za masika na el nino, zinazoendelea kunyesha nchini na kusababisha mafuriko.

Pia anasema mlundikano wa taka husababisha taka hizo kuoza na kusababisha harufu mbaya, harufu hiyo inaweza kuwa na sumu na hiyo ni kutokana na aina ya taka zenyewe.

"Mbali na athari za kiafya katika mapafu ya binadamu, pia kuna taka za plastiki hizi ni hatari kwani hazioz, lakini zikipigwa sana na jua kupasuka na kukatika vipande vipande na kwa kuwa maeneo ya kuhifadhia taka yapo kwenye makazi ya watu hivyo vipande vinaweza kuwachoma mtu hasa watoto na kusababisha jeraha,"anasema Lubeya.

Dk. Lubeya anatoa uongozi wa Manispaa Morogoro kuzingatia sheria ya mazingira ya mwaka 2004, inayotaka kuzoa taka mara kwa mara ikiwa ni pamoja na kuweka uzio sehemu iliyotengwa, kwa ajili ya kuhifadhi taka kwa muda ili kuepuka madhara yatokanayo na mlundikano wa taka.

Kwa upande wake Manispaa ya Morogoro Ndimile Kilatu, anasema kwamba sheria ya afya ya jamii ya mwaka 2009 inazuia mlundikano wa taka kwa muda mrefu, kwani mlundikano huo unasababisha athari kwa jamii kiafya, ambapo amesema wote waliopewa jukumu la kusimamia usafi wa mazingira kufanya kazi kwa kuzingatia sheria ya mazingira ya hiyo.

Kilatu anasema kitendo cha mlundikano wa taka katikati ya watu ni hatari, kwani kunaweza kusababisha madhara kwa jamii kama vile magonjwa ya milipuko ikiwemo vifo, hivyo idara zilizipewa kujumu la kusimamia sheria hizo zinatakiwa kuhakikisha mazingira yanakuwa safi kila siku.

Meya wa Manispaa hiyo Pascal Kihanga, anasema atahakikisha anafanya kila liwezekanalo ili kuhakikisha sheria ya mazingira ya mwaka 2004 inafuatwa, kikamilifu ili kuondoa kero ya mlundikano wa taka maeneo mbalimbali ya manispaa hiyo.